

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM  
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI  
DAR ES SALAAM**

---

**MATANGAZO YA DOMINIKA YA 27  
MWAKA C TAREHE 2 OCTOBA, 2022.**

**Kristo.....**

**MCHANGO WA PILI**

Kwa ajili ya **MIITO YA KITAWA**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

**NDOA**

Bw.Paulo Samson Marwa Mtoto wa Samson Chacha na Christina Matinde na Bi.Pendo Joseph Siong'o Mtoto wa Joseph Siong'o na Rhobi Ngoko.  
Tangazo la Kwanza.

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

**MTIHANI WA SEMINARI**

Kwa wale vijana wa darasa la saba waliofaulu mthani wa mahojiano watafanya mthani wa pili kwa masomo ya hisabati, maarifa ya jamii, Sayansi na Dini Jumamosi ya tarehe 08/10/2022 Msimbazi Centre saa 3:00 Asubuhi.

**HIJA YA KITAIFA YA MAMA BIKIRA MARIA**

Kutakuwa na Hija ya Kitaifa ya Mama Bikira Maria itakayofanyika katika kituo cha Hija Mbeya kuanzia tarehe 9/10 -14/10, 2022. Hija itaongozwa na Askofu mkuu Jimbo la Mbeya Askofu Gervas Nyaisonga na Askofu Libena wa Jimbo la Ifakara. Gharama kwa kila mshiriki ni shilingi 200,000 ambayo itajumuisha nauli, chakula na malazi kwa siku zote nne. Wote mnakaribishwa. Kwa maelezo Zaidi wasiliana na uongozi wa H/Walei Parokia.

**UCHAGUZI WA VIONGOZI WA HALMASHAURI YA WALEI KATOLIKI**

Jana Tarehe 01/10/2022 Uchaguzi ulifanyika kwa Jumuiya za Mt. Maria Goreti, Marcelino, Veronika, Joakimu, Yohane Bosco, na Familia Takatifu. Jumamosi ijayo tarehe 8/10/2022 ni zamu ya jumuiya zilizobaki ambazo ni Mt. Petro, Mikael, Yuda Thadei, Martin de Porres, Faustina, Yohane Vianney, Maria Magdalena na Stephano Shahidi. Wasimamizi mnaombwa kuja kuchukua makabrasha ya uchaguzi mara baada ya Misa ofisi ya H/walei.

**HIJA UWAKA JIMBO**

Uongozi wa uwaka Parokia unawaomba viongozi wa Jumuiya kuratibu zoezi la kuandikisha mahujaji tarehe 14/10/2022 huko visiga kwa masista wa dada wadogo. Mwisho wa kuwasilisha majina utakuwa jumapili tarehe 9/10/2022 saa 12 jioni.

**ST GASPER VOCATION TRAINING**

Wamisionari wa Shirika la Damu Aziz ya Yesu wanatangaza nafasi za masomo katika chuo chao cha Mt. Gaspar kwa fani za Electrical Installation, Information

Technology, Motor vehicle Mechanics, Carpentry, Tailoring and design, Catering, Driving na English course kwa maelezo Zaidi fika ofisi ya H/walei Parokia.

### **SHUKRANI**

Utoto Mtakatifu Parokia wanatoa shukrani zao za dhati kwa Baba Paroko, Kamati Tendaji na wazazi kwa kufanikisha kukabidhi mshumaa wa utoto katika Parokia ya Madale. Jumla ya Watoto na walezi walioshiriki walikua 65. Wanaomba Jumuiya ziendelee kujitoa katika kufanikisha Hija ya Mafia. Hija hiyo ni tarehe 6/10/2022 mpaka 10/10/2022.

### **HUDUMA KANISANI**

Leo tunahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Maria Alakok Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Yohane Paul ii. Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Teresia wa Mtoto Yesu wajiandae

### **MAUZO**

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu. Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem.